HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA VIWANDA VIDOGO VIDOGO KWA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM, MHESHIMIWA PAUL MAKONDA, KATIKA UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI LA VIWANDA VIDOGO VIDOGO VINAVYOJENGWA NA HALMASHAURI YA JIJI KATIKA ENEO LA KARAKANA YA MWANANYAMALA, DAR ES SALAAM

TAREHE 09 SEPTEMBA, 2017

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipanga na kusisitiza Mamlaka zake na wadau wa maendeleo kuanzisha viwanda nchini kwa lengo la kufikia uchumi wa kati. Kwa kuzingatia Kauli Mbiu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli inayochochea uanzishwaji wa viwanda hivyo nchini Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, pamoja na kuwawezesha wawekezaji wakubwa wa viwanda kufikia malengo yao na kuwajengea mazingira bora ya uwekezaji, imepanga kujenga viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya wanawake, vijana na walemavu wa Jiji la Dar es Salaam pamoja na kuwapatia fedha za mikopo zinayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

2. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilitenga kiasi cha shilingi 200,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo ambao utekelezaji wake ulianza tarehe 01 Juni, 2017 ambapo hadi kufikia mwezi Agosti, 2017 ujenzi wa miundombinu hiyo umefikia asilimia 95. Gharama za mradi huo ni shilingi 199,988,052.00. Ujenzi huo utaendelea kutekelezwa na Halmashauri ya

Jiji katika Manispaa za Ilala, Kigamboni, Temeke na Ubungo kwa kadri maeneo yatakavyopatikana.

3. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

Ujenzi wa miundombinu ya viwanda hivyo umepangwa kutekelezwa katika awamu mbili na ujenzi wa miundombinu iliyopangwa katika mradi huu ni kama ifuatavyo:

Na.	Miundombinu	Idadi
(a)	Ujenzi wa majengo ya viwanda vidogo vidogo (Micro Industries)	18
(b)	Ujenzi wa majengo ya viwanda vidogo vidogo (Small Industries)	04
(c)	Ujenzi wa Mgahawa wa Chakula (Canteen)	01
(d)	Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Utawala na Ukumbi wa Mikutano	01
(e)	Ujenzi wa kibanda cha Mlinzi	01
(f)	Ujenzi wa vyoo vya umma vya kulipia (matundu 10)	01
(g)	Ujenzi wa vyoo vya umma kwa matumizi ya ofisi/wajasiriamali (matundu 4)	01
(h)	Ujenzi wa eneo la maegesho ya magari (car parking) na maboresho ya bustani, maua na miti (landscaping)	01

4. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

Miundombinu iliyojengwa katika awamu hii ya kwanza ni kama ifuatavyo:

Na.	Miundombinu	Idadi
(a)	Ujenzi wa majengo ya viwanda vidogo vidogo (Micro Industries) yenye vyumba vitatu (3) kila moja	02
(b)	Ujenzi wa vyoo vya umma kwa matumizi ya ofisi/wajasiriamali (matundu 4), mashimo ya maji machafu (Soak pit and Soak away pit)	01
(c)	Ujenzi wa lango la kuingilia katika viwanda	01

5. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaona kuna kila sababu ya kuendelea kuwasaidia wanawake, vijana na walemavu wanaopata mikopo kutoka Halmashauri ya Jiji kwa kuwa mazingira wanayofanya shughuli

zao sio rafiki na wanahangaika sana kutafuta masoko. Hivyo, Mipango ya Halmashauri ya Jiji ni kuendelea kujenga viwanda hivyo katika maeneo mbalimbali katika Jiji ili kuisaidia Serikali katika juhudi zake za kufikia uchumi wa kati

UZALISHAJI NA MAFUNZO

1. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Kutokana na mikopo inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri, jumla ya vikundi sita (6) vya wanawake, vijana na walemavu vyenye jumla ya wanachama 82 vipo tyari kuanza shughuli zao katika eneo hili la viwanda vidogo vidogo. Wajasiriamali hao wamepanga kuzalisha chaki, kusindika vyakula, ushonaji, utengenezaji wa batiki, sabuni na mikate. Shughuli nyingine watakazozifanya ni kutengeneza dawa za usafi, sabuni na kushona viatu.

2. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo inashirikiana na Shirika la Kukuza Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) kuwajengea uwezo wajasiriamali hao itawawezesha kupata mafunzo yatakayowasaidia kuboresha zaidi uzalishaji na biashara zao. Kwa upande mwingine itakuwa rahisi zaidi kwao kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha, wadau mbalimbali pamoja na huduma muhimu kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa Nchini (TFDA) na wadau wengine.

3. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Kwa kuwawezesha wajasiriamali hao kufanya kazi katika eneo moja linaloeleweka itarahisisha ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo na udhibiti wa fedha za Serikali zinazotolewa kufanikisha malengo ya wajasiriamali hao.

UPATIKANAJI WA MASOKO

1. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Kwa kushirikiana na taasisi za Serikali, mashirika ya umma, wadau wa ndani na nje ya nchi pamoja na mahusiano yetu ya miji mingine ya nchi za nje, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam itawasaidia wajasiriamali hao kujitangaza zaidi ili waweze kupata masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi. Vile vile wataweza kubadilishana ujuzi na wenzao wa maeneo mengine, kufundishana wenyewe kwa wenyewe, kusaidiana na kupeana maarifa ya kutengeneza na kuuza bidhaa zao pamoja na ziara za mafunzo kulingana na uhitaji.

2. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Halmashauri ya Jiji imetenga jumla ya Shilingi 977,000,000.00 kwa ajili ya kuendelea kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na walemavu pamoja na kujenga viwanda vidogo vidogo vingine katika maeneo tuliyoyataja hapo juu, hivyo Halmashauri ina jukumu kubwa la kuvitangaza viwanda hivyo ili wajasiriamali hao wafanikiwe kupata masoko na kunufaika na kazi za mikono yao.

MWISHO

1. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**

   Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam itaendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano katika juhudi zake za kuwa na Tanzania ya Viwanda na kufanikiwa kufikia uchumi wa kati. Tutafanya hivyo kwa kuzingatia Sera ya Tanzania ya Viwanda ambayo ni mkakati uliopo katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), MKUKUTA II, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na kauli mbiu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe magufuli ya kuwa na Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati.

2. **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,** naomba kuwasilisha